**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI**
SHULE YA SEKONDARI MALANGALI S.L.P 4, **MALANGALI.**

**Kumb. Na. U. 19/Vol.V.II/ 222**
**Ndg ………………………………….**
**………………………………………**
**………………………………………**

**YAH: MAAGIZO NA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026.**

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule hii. Nakupongeza sana kwa kuchaguliwa na nategemea utaitumia nafasi hii ipasavyo ili kujenga historia nzuri ya maisha yako. Ni mategemeo ya shule kuwa uwapo hapa utashirikiana vizuri na walimu, Watumishi wasio walimu na wanafunzi wenzako kufanya kazi za darasani na nje ya darasa. Unatakiwa kufika shuleni tarehe **05/01/2026** ili kuanza masomo yako kikamilifu na kwa wakati.

**MAHALI SHULE ILIPO NA NAMNA YA KUFIKA SHULENI**
Shule ipo Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Mufindi, Tarafa ya Malangali na Kata ya Malangali. Ukitokea Mafinga au Makambako kwa kufuata barabara kuu itokayo Dar es salaam kwenda Mbeya, Shukia kituo cha mabasi kiitwacho Mbalamaziwa, hapo utapata usafiri wa kuja Malangali sekondari umbali wa kilometa 18 Magharibi mwa Mbalamaziwa.

**1.0 SARE ZA SHULE**
1.1 Shati mbili nyeupe kabisa tetron au Polista, zenye ukosi wa kawaida, mikono mifupi pamoja na tai mbili nyeusi na dark bluu.
1.2 Suruali ya dark blue moja na nyeusi moja upana wa chini uwe wa inchi 16-18, iwe na rinda mbili kila upande na mifuko mitatu, mkanda wa kuvalia suruali uwe wa ngozi rangi nyeusi (chuma cha kwenye mkanda kisiwe na urembo na maandishi ya aina yoyote,pia usiwe utambi).
1.3 Viatu vyeusi jozi mbili, visiwe buti, viwe vya kamba. Viatu visivyofungwa na kamba havikubaliki/haviruhusiwi.
1.4 Jozi mbili za soksi nyeusi
1.5 Fulana moja ya kijivu yenye kola (T- shirt).Ukishindwa kuipata huko utaipata jirani na shule kwa Tsh. 15,000/=
1.6 Sweta nadhifu la bluu lenye shingo ya V
1.7 Track suti nyeusi yenye mikanda ya rangi nyeupe mikononi
1.8 Raba nyeupe au viatu kwa ajili ya michezo.
1.9 Jezi ya michezo rangi nyeusi (Bukta na Tshirt).Isiwe na jina la timu yoyote
1.10 Shati moja rangi ya bluu bahari na suruali moja (rangi ya khaki) kwa ajili ya kuvaa baada ya vipindi vya darasani**. (**Vipimo viwe sawa na sare za darasani**).**
**NB : Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuja shuleni na nguo za nyumbani tofauti na zilizoagizwa.**

**2.0 VIFAA VYA MALAZI**
2.1 Blanketi 1, shuka mbili za rangi ya pinki na mto wenye foronya ya rangi ya pinki

2.2 Godoro lenye upana wa futi mbili na nusu.( Lishonewe Foronya isiyopitisha maji) material ya foronya ni ya seat cover)
2.3 Chandarua (Mosquito net) kwa ajili ya kujikinga na malaria.
2.4 Truncker /sanduku la chuma la kuhifadhia vifaa vyako uwapo shuleni

**3.0 VIFAA VYA CHAKULA**
3.1 Kontena, Kikombe na Kijiko.

**4.0 VIFAA VYA TAALUMA**.
4.1 Daftari kubwa (Counter books) zisizopungua 12, mathematical set na peni za kutosha.
4.2 **Spring file 2**, moja ndani yake kuwe na kivuli cha cheti cha kuzaliwa, fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule, hati ya mganga iliyojazwa baada ya kupimwa.
4.3 Karatasi bando mbili A4 ( Ream Paper 2)

**5.0 AFYA**
5.1 Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko(kwa ajili ya usafi binafsi), mopa moja(squizer) kwa ajili ya usafi, toilet paper bunda 05.
5.2 Matibabu ni juu ya mzazi/mlezi (**aje na kadi ya bima ya afya kwa ajilli ya matibabu**. (Endapo hana bima ya afya aje na shilingi 50,400 ili akatiwe bima ya **NHIF** ili iwe rahisi kupata matibabu endapo ataugua.).
5.3. Kwa ajili ya kujikinga na magonjwa ya ngozi miguuni na sehemu za siri aje na taulo na nguo za ndani za kutosha.

**6.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**
6.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978.
Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.
Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.
Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

(a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule ndani na nje ya shule ni muhimu
(b) Kutimiza kwa makini maandalio ya siku (Preparation) na siku za mwisho wa wiki.
(c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
**(h) MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI AU KUTUMIA SIMU KIPINDI CHOTE AWAPO SHULENI.**

**6.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI**.

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga

3. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya.kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
4. Uvutaji bangi na sigara
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoa/kusababisha mimba
10. Kulawiti
11. Utoro
12. Kutofanya mazoezi au mitihani ya masomo na kutega vipindi
13. Kiburi na ukaidi
14. Kugoma/kuchochea na kuongoza mgomo
15. Kukataa adhabu kwa makusudi
16. Kumiliki/kutumia simu shuleni

**TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU. NAKUTAKIA SAFARI NJEMA NA KARIBU SANA MALANGALI SEKONDARI**.


**……………...**
**1. MWL.OSCAR B. MWANUKE (0765386659)**
**MKUU WA SHULE**
**2. MWL.SHAFII B. HARIDI (0745311293)**
**MAKAMU MKUU WA SHULE**
**3. MWL.SIFA H. KHERY (0746580233)**
**MWANDAMIZI MALEZI.**

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MUFINDI DISRICT COUNCIL
MALANGALI SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officers in a recognized Hospital in respect of all new entrants of Malangali Secondary School

Full Name……………………………………………………………………………………………….
Age…………………………………………………………………………………………………….
1. Blood comment (red & white)……………………………………………………………….

3. Urine examination………………………………………………………………………..

4. Stool examination…………………………………………………………………………

5. Syphilis test………………………………………………………………………………

6. T.B. test…………………………………………………………………………………….

7. Ear test……………………………………………………………………………………

8. Spleen………………………………………………………………………………………

9. Abdominal ………………………………………………………………………………….

10. Eye test……………………………………………………………………………………

11. Additional information or any other physical, hereditary or infectious diseases
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

Treatment after examination
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
………………………………….........................................................................

**MEDICAL CERTIFICATE**

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue for further education

Signature…………………………………………………………………………………
Designation………………………………………………………………………………
Station……………………………………………………………………………………
Official stamp……………………………………………………………………………
Date………………………………………………………………………………………

**N.B Fomu hii ijazwe na Mganga katika Hospitali inayotambulika na serikali.**

**KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI**

PICHA

A. MWANAFUNZI NA MZAZI/ MLEZI

i. Jina la mwanafunzi……………………………………………

ii. Tarehe ya kuzaliwa………………………..mahali…………………

PICHA

iii. Jina la Baba………………………………yu hai/ amefariki…………

iv. Mahali anakoishi; kijiji/mji……………………kata…………………tarafa………

v. Kazi ya Baba …………………………………

vi. Anuani yake………………simu ………………………

PICHA

vii. Jina la Mama……………………………………

viii. Kazi ya Mama…………………………………

ix. Anuani yake………………………simu…………………

x. Mahali anapoishi; kijiji/Mji…………....kata…………………tarafa……………

PICHA

xi. Jina la mlezi 01…………………………………..

xii. Kazi yake…………………………………….

xiii. Mahali anapoishi; kijiji/ Mji……………kata……………tarafa…………......

xiv. Anuani yake……………………simu…………………………

PICHA

Jina la mlezi 02…………………………………..

Kazi yake……………………………………

Mahali anapoishi; kijiji/ Mji……………kata……………tarafa…………......

Anuani yake……………………simu…………………………

B. AHADI YA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE (MWANAFUNZI)

Mimi...................................................................................................................

Naahidi kufuata sheria,kanuni na taratibu za shule hii na kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakaokuwa ndani na nje ya shule. Sitajihusisha na migomo, fujo, wala makosa ya jinai.

Saini.............................................Tarehe...........................................

C. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi ....................................................................................................................ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi aliyeweka ahadi hapo juu, naahidi kumpatia michango mbalimbali na mahitaji yote yanayotakiwa kujiunga na shule hii.

Saini.................................................................Tarehe...........................................